# MKATABA WA UTOAJI HUDUMA KWA WANANCHI

## Huduma kwa Wakenya na UNESCO

unesco

Kenya National Commission

## DIRA

Shirika linaloongoza katika kuendeleza amani, maendeleo endelevu, na ushirikiano wa kitaaluma katika maeneo ya ustadi ya UNESCO.

## DHAMIRA

Kukuza ujenzi wa amani, maendeleo endelevu, na ushirikiano wa kitaaluma kupitia maeneo ya UNESCO ya elimu, sayansi, utamaduni na mawasiliano na habari.

## MAADILI MSINGI

Uadilifu | Utaaluma | Ushirikiano | Ubora katika utoaji wa huduma | Adabu | Uaminifu kwa sheria

## SISI NI NANI

Tume ya Kitaifa ya Kenya ya UNESCO ni shirika la serikali lililoanzishwa na Sheria ya Bunge (Sheria ya KNATCOM, 2013) ili kukuza ushirikiano kati ya UNESCO na Kenya na kutekeleza programu katika maeneo ya ustadi ya UNESCO.

| HUDUMA INAYOTOLEWA | MAHITAJI YA MTEJA | MALIPO | MUDA WA KUHUDUMIWA |
|---|---|---|---|
| Kujibu maswali ya jumla | Maswali yaliyoandikwa Baruapepe, barua | Hamna | Katika muda wa siku mbili (2) za kazi |
| | Simu, uso kwa uso | Hamna | Mara moja |
| Usuluhishaji wa malalamiko | Fomu ya malalamiko ya mteja iliyojazwa, baruapepe, barua, masanduku ya malalamiko, simu | Hamna | Thibitisha kupokea katika muda wa siku (2) za kazi<br>Suluhisha katika muda wa siku kumi na nne (14) za kazi |
| Kuendesha ukuzaji wa uwezo katika maeneo ya ustadi ya UNESCO katika elimu, sayansi asilia, sayansi ya kijamii na ubinadamu, utamaduni na, mawasiliano na habari. | Mahitaji ya uwezo, ombi la mteja, mpango wa KNATCOM | Hamna / kugawana gharama | Kila wakati/jambo linaloendelea |
| Kusambaza wito wa zawadi, tuzo, ufadhili wa masomo, udhamini wa uanazuoni na ruzuku za masomo ili kuhakikisha Wakenya wanafahamu uwepo wake, wanazifikia na wanazitumia. | Mpango wa KNATCOM, ombi la mteja | Hamna | Kila wakati/jambo linaloendelea na katika muda uliowekwa |
| Utafiti na utoaji ushauri katika maeneo ya ustadi ya UNESCO | Ombi la mteja, mpango wa KNATCOM | Kulingana na makubaliano ya mkataba | Kila wakati/Jambo linaloendelea |
| Kuchapisha makala za utafiti katika Jarida la KNATCOM | Wasilisha miswada inayotimiza mahitaji | Hamna /kugawana gharama | Mara mbili kwa mwaka |
| Vifaa vya Kituorasilimali cha KNATCOM kwa madhumuni ya elimu na utafiti | Jisajili katika Kituorasilimali | Hamna | Hufunguliwa:<br>Saa mbili asubuhi hadi saa saba mchana na kutoka saa nane mchana hadi saa kumi na moja jioni siku za kazi pekee |
| Ununuzi wa bidhaa na huduma | Zingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi na Utupaji Mali ya Umma ya 2015 | Kama Sheria hiyo inavyoelekeza | Wagavi/watoa huduma wahitimu kimbele kila baada ya miaka miwili<br>Nunua kulingana na Mpango wa Ununuzi wa Mwaka Ulioidhinishwa na jinsi Sheria ya PPAD, 2015 na Kanuni ya 2020 zinavyoelekeza. |
| Malipo ya bidhaa na huduma | Toa hati za kuthibitisha | Hamna | Malipo kutolewa katika muda wa siku 30 baada ya kupokea hati zote za uhasibu |

## UTARATIBU WA MALALAMIKO

Iwapo hujaridhika na huduma zetu unaweza kuwasilisha malalamiko kwa afisa aliyekuhudumia mara ya kwanza, kuweka malalamiko yako yaliyoandikwa kwenye sanduku la malalamiko/pongezi la KNATCOM na/au kulalamika zaidi au kata rufaa kwa:

### KATIBU MKUU/AFISA MKUU MTENDAJI

Tume ya Kitaifa ya Kenya ya UNESCO
Jengo la Benki ya Taifa Ghorofa ya 16
(Barabara ya Harambee)
S.L.P. 72107 - 00200 NAIROBI

+254 (0) 20 2229053
www.unesco.go.ke
sg@unesco.go.ke
NatcomUnescoke
NatcomUnescoKe

**AU**

### MWENYEKITI

Tume ya Utekelezaji wa Haki
West End Towers
Ghorofa ya Pili, Waiyaki Way
S.L.P. 20414 – 00200, NAIROBI

+254 (0) 20 227000 / 2303000 / 26 03765
www.ombudsman.go.ke
info@ombudsman.go.ke
complain@ombudsman.go.ke

KENYA VISION 2030

SUSTAINABLE DEVELOPMENT GOALS

ISO 9001-2015 Certified